**MAELEZO YA MWENYEKITI WA TUME YA UTUMISHI WA UMMA WAKATI WA UFUNGUZI WA MAFUNZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA [SURA YA 298, MAREJEO YA MWAKA 2019] NA OPRAS KWA WATUMISHI WA KADCO, YALIYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KADCO-KIA, KILIMANJARO, TAREHE 10 MEI, 2021**

- *Dkt. Natu E. Mwamba, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Uendelezaji Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro (KADCO),*
- *Bibi Christine G. Mwakatobe, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji KADCO,*
- *Wawezeshaji kutoka Ofis ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma,*
- *Menejimenti ya KADCO,*
- *Washiriki wote,*
- *Waandishi wa Habari ,*
- *Wageni waalikwa,*
- *Mabibi na Mabwana;*

***"Ninawasalimia katika Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"***

***Awali ya yote***, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na kutuwezesha kukusanyika hapa leo ili kushiriki katika mafunzo haya muhimu sana.

Aidha, kwa namna ya kipekee, nampongeza Dkt. Natu E. Mwamba kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Uendelezaji Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro (KADCO) na ninamtakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yake haya mapya. Vilevile naomba tuchukue dakika moja ya kukaa kimya ili tumuombee ndugu yetu Bw. Gregory G. Teu aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya KADCO ambae ametangulia mbele za haki,

(***Raha ya Milele Umpe ee Bwana na mwanga wa Milele umwangazie. Apumzike kwa Amani……Amina!)***

***Kwa upande mwingine***, naipongeza Menejimenti ya KADCO chini ya Bibi Christine G. Mwakatobe kwa kuandaa mafunzo haya kuhusu Utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 na OPRAS kwa Watumishi wa KADCO ambayo naamini

yataboresha utendaji kazi wenu na uzingatiaji wa sheria wakati wa ushughulikiaji wa haki na wajibu wenu na wa wengine wakati wa utoaji wa huduma katika uwanja wetu wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA).

***Ndugu washiriki***

Naomba mniruhusu sasa nizungumze kuhusu Tume ya Utumishi wa Umma na majukumu yake pamoja na jukumu hili la leo la uwezeshaji. Tume ya Utumishi wa Umma imeundwa chini ya Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, Tume ilianza kufanya kazi rasmi tarehe 07 Januari, 2004 baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteua Viongozi kusimamia utendaji wake.

***Ndugu washiriki,***

Kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, kikisomwa kwa pamoja na Aya ya 14(1) ya Taratibu za Uendeshaji za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Tume ya Utumishi wa Umma inaundwa na Mwenyekiti na Wajumbe Sita ambao wote huteuliwa na Rais. Kwa sasa Tume ina Wajumbe wafuatao:-

1. Mheshimiwa Jaji (Mstaafu), Dkt. Steven J. Bwana - Mwenyekiti
2. Bw. George D. Yambesi - Mjumbe
3. Balozi (Mstaafu) John M. Haule - Mjumbe
4. Balozi (Mstaafu) Daniel Ole Njoolay - Mjumbe
5. Alhaj Yahya F. Mbila - Mjumbe
6. Bibi Khadija A. Mohamed Mbarak - Mjumbe
7. Bibi Immaculate P. Ngwale - Mjumbe

***Ndugu washiriki,***

Majukumu ya Tume yameainishwa katika Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, sura ya 298. Majukumu hayo ni pamoja na:-

i. Kumshauri Rais kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yake aliyopewa Kikatiba chini ya Ibara ya 36 kuhusu ujazaji wa nafasi zilizo wazi katika Utumishi wa Umma kadri Rais atakavyohitaji;

ii. Kumshauri Rais kuhusu masuala ya utumishi kadri atakavyohitaji;

iii. Kutoa miongozo na kufuatilia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma;

iv. Kupokea na kushughulikia rufaa za mashauri yaliyotolewa maamuzi na Mamlaka za Nidhamu;

v. Kuwezesha, kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wa watumishi wa Umma wa ngazi mbalimbali ili uwe wa ufanisi na wenye kuzingatia matokeo (result oriented);

vi. Kuwaita Watendaji Wakuu kutoa maelezo kuhusu utendaji kazi usioridhisha pale Tume inapokuwa na ushahidi au malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu;

vii. Kuhakikisha kuwa Taratibu za Uendeshaji za Utumishi wa makundi mbalimbali zinatayarishwa na kutumika ipasavyo;

viii. Kuwachukulia hatua kupitia Mamlaka zao za Nidhamu Watendaji Wakuu watakaoshindwa kuwachukulia hatua watumishi walio chini yao kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu zinazosimamia utendaji kazi katika Utumishi wa Umma;

ix. Kutekeleza majukumu mengineyo kwa mujibu wa Sheria mbalimbali zilizopo.

***Ndugu washiriki,***

Kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma Toleo la mwaka 2008, wajibu mkubwa wa usimamizi wa watumishi umebaki mikononi mwa kila Mamlaka ya Ajira na Mwajiri. Sheria ya Utumishi wa Umma imewapa Watendaji Wakuu dhamana na Mamlaka ya kusimamia Rasilimali Watu walio chini yao katika maeneo ya Ajira, Upandishwaji vyeo, Uendelezaji wa Watumishi kwa njia ya mafunzo, Tathmini ya utendaji kazi, Likizo ya mwaka, Likizo ya ugonjwa, Likizo ya uzazi, Uchukuaji wa hatua za nidhamu, Kustaafu na kuacha kazi kwa mujibu wa Sheria.

Kwa msingi huo, Waajiri na Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu zitapaswa kutekeleza yafuatayo:-

i) Kusimamia na kutekeleza kikamilifu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusu masuala ya Rasilimali Watu.

ii) Kuimarisha na kuboresha Mifumo ya Utunzaji wa Kumbukumbu za kiutumishi ili waweze kufanya maamuzi sahihi na kuwahudumia vyema watumishi wao.

iii) Kuwasilisha taarifa Tume kwa wakati na kwa kuzingatia Mwongozo wa Tume wa kuwasilisha taarifa mbalimbali zinazotakiwa kwa maamuzi.

iv) Kuandaa Mpango wa mafunzo unaotokana na tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kuutekeleza. Mafunzo yanawawezesha watumishi walio chini yao kuzifahamu Sheria, Kanuni na Taratibu za kiutumishi ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa Sheria.

v) Kuhakikisha Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) unatekelezwa ipasavyo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

vi) Kusimamia na kuzingatia kwa ukamilifu Maadili ya kazi.

***Ndugu washiriki,***

Ili kuhakikisha masuala haya ya usimamizi wa Rasilimali Watu yanazingatiwa ipasavyo, Tume kupitia jukumu lake la urekebu inatumia mikakati ifuatayo :-

- ✓ Inatoa Miongozo ya masuala ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma kama vile Mwongozo wa Masuala ya Ajira katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2011; Mwongozo wa Ushughulikiaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2011 n.k

  Miongozo hii inatoa ufafanuzi na maelekezo ya hatua muhimu za kufuata katika utekelezaji wa masuala ya ajira na nidhamu katika usimamizi wa Rasilimali watu.

- ✓ Kufanya ukaguzi wa kawaida wa uzingatiaji taratibu katika usimamizi wa Rasilimali Watu na kufanya ukaguzi maalum kufuatia malalamiko ya watumishi au maelekezo kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi au Katibu Mkuu UTUMISHI.
- ✓ Waajiri wanawajibika kuwasilisha Tume ya Utumishi wa Umma taarifa za utekelezaji wa usimamizi wa Rasilimali Watu katika Taasisi zao. Taarifa hizo zinaiwezesha Tume ya Utumishi wa Umma kuandaa na kuwasilisha Taarifa ya hali ya Utumishi wa Umma nchini kwa kipindi cha mwaka husika kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Ndugu washiriki,***

Naomba nichukue fursa hii kuwaasa ***mfanye kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma kwa kufanya kilicho sahihi huku mkizingatia Utaalamu***, ***Uaminifu na Uwajibikaji katika Utendaji kazi wenu wa kila siku wakati wa utoaji huduma katika uwanja wetu wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA).***

***Ndugu washiriki,***

Wote tunafahamu kuwa hakuna Haki isiyo na Wajibu. Kwa upande mmoja, Waajiri wana wajibu wa kuhakikisha watumishi wanapata stahili zao zote za kiutumishi ambazo ni haki yao, na kwa upande wa pili, watumishi wana wajibu wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma ambayo ni haki ya Waajiri. Hivyo, ni muhimu kwa watumishi kupandishwa vyeo, kuthibitishwa kazini na kulipwa stahili zao mbalimbali kwa wakati na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Aidha, Watumishi wa Umma wana wajibu wa kufanya kazi kwa bidii, weledi, uaminifu, uadilifu na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma ili kupata stahili zao.

***Ndugu washiriki,***

Utendaji kazi wenu wa kila siku ni lazima utathminiwe ili kutimiza malengo ya Taasisi pamoja na malengo ya mtumishi mmoja mmoja. Wote tunafahamu kuwa suala la ujazaji wa OPRAS ni la kisheria kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1)(a)(ii) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, kikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 22 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Hata hivyo, watumishi wengi

wamekuwa hawajazi kabisa OPRAS au wamekuwa wakijaza kwa mazoea tu bila kuzingatia vipindi vya ujazaji, kuwa na malengo ya utendaji kazi yasiyo “SMART” na kutokujaza fomu za OPRAS kwa ukamilifu. Kupitia mafunzo haya, ninaamini kila mtumishi atapata uelewa wa kutosha wa jinsi ya kujaza OPRAS na hatimaye kufanyiwa tathmini ya utendaji kazi wake kama sheria inavyoelekeza.

***Ndugu washiriki,***

Nichukue fursa hii pia kuwakumbusha kuhusu suala la Utunzaji wa Siri. Katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia mmomonyoko mkubwa wa maadili kwa baadhi ya Watumishi wa Umma kuvujisha siri za Serikali. Aidha, wapo watumishi wanaotumia mitandao ya kijamii kinyume na maadili ya Utumishi wa Umma. Ninawasihi watumishi wote wa Umma kuzingatia viapo vyenu vya Maadili ya Utumishi wa Umma kwa ustawi wa nchi yetu.

***Ndugu washiriki,***

Kwa kuhitimisha na kwa kutambua umuhimu wa mafunzo haya, ninawaomba mshiriki kikamilifu katika mafunzo yatakayofanyika hapa kwa muda wa majuma mawili kuanzia tarehe 10/05/2021 hadi 24/05/2021. Ni imani yangu kuwa Mafunzo haya yataongeza tija katika usimamizi wa majukumu na utoaji wa mrejesho wa utekelezaji wa majukumu hayo kwa Taasisi na mtumishi mmoja mmoja sawa na kuongeza uelewa na hatimaye uzingataji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi katika ushughulikiaji wa haki na wajibu wa watumishi wa KADCO.

*“Ba**ada ya kusema hayo, natamka kuwa mafunzo yamefunguliwa rasmi”***

***AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA***